Pg 21

# Serikali yapeleka mwendokasi 20 ya majaribio Mbagala-Gerezani

Na Rehema Lugono

SERIKALI imesema imepeleka mabasi yaendayo haraka zaidi ya 20 yafanye majaribio katika njia ya barabara ya Kilwa itokayo Mbagala kwenda Gerezani.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amesema mabasi 151 yameshafika nchini kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri kwa njia hiyo pekee.

Chalamila alisema baadhi ya mabasi hayo yameazimwa kwa ajili ya kupunguza changamoto ya usafiri katika Barabara ya Kimara ambayo itakuwa na mabasi zaidi ya 171.

"Maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan yalikuwa ili kuleta ufanisi wa mabasi hayo ni vyema kila barabara ikapewa kampuni moja yenye ufanisi kwa ajili ya kuongeza kiwango cha ushindani, aliyekuwa anatoa huduma Kimara, Mbezi hadi Gerezani alikuwa ni UDART na sasa atakayekuja kutoa huduma ni TransDar," alisema.

Aliongeza: "Barabara ya Kilwa atatoa huduma MOFAT, wakati huohuo barabara ya kuelekea Airpot na nyingine za kwenda Tegeta kampuni zingine zitatoa huduma".

Chalamila alisema kiwango cha kero za huduma za mabasi hayo zimeanza kupungua, hivyo amepiga marufuku vyombo vingine vya usafiri zikiwemo bodaboda, bajaji na magari binafsi kupita katika njia ya mwendokasi.

Awali alisema siku chache zilizopita walishuhudia baadhi ya Watanzania wakipaza sauti wakilalamikia huduma mbovu, uchache na uchakavu wa mabasi ya mwendokasi.

Chalamila alisema kupitia timu maalumu ya usimamizi wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa changamoto hizo zimetatuliwa.

Alisema baadhi ya changamoto zilizotatuliwa ni mabasi zaidi ya 50 kupelekwa kutoa huduma kwa kushirikiana na mabasi ya UDART kwa Barabara ya Kimara-Gerezani hadi Kivukoni.

CamScanner